THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF WORKS AND TRANSPORT
TANZANIA SHIPPING AGENCIES CORPORATION
TASAC

*In reply please quote*

**Ref. No.**: EA/121/365/01/118

**Date:** 27th June, 2022

Executive Secretary,
Tanzania Shippers Council,
**DAR ES SALAAM.**

Executive Secretary,
Tanzania freight Forwarders Association (TAFFA),
**DAR ES SALAAM.**

**All Licensed Shipping Agents.**

**RE: GOVERNMENT NOTICE ON INLAND CLEARANCE DEPOT TARIFF**

Kindly refer to the captioned subject matter.

2. A Government Notice No 459 on approved tariff for Inland Clearance Depot (ICDs) was published on 24th June, 2022.

3. The Order is attached for your reference and compliance.

4. Thanking you for your cooperation.

Kaimu Abdi Mkeyenge
**DIRECTOR GENERAL**

PPF Tower Building 7th and 8th Floor, Plot No. 20/21, Garden Avenue/Ohio Street,
P. O. Box 989, Dar es Salaam - Tanzania, Tel: +255 222 127 314, Fax: +255 222 127 313,
Email: dg@tasac.go.tz, info@tasac.go.tz, Website: www.tasac.go.tz

TAMKO LA SERIKALI NA. 459 la tarehe 24/6/2022

SHERIA YA UWAKALA WA MELI TANZANIA,
(SURA YA 415)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 28(3)*

AMRI YA TOZO ZA BANDARI KAVU, 2022

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Tozo za Bandari Kavu, 2022 na itaanza kutumika siku thelathini baada ya tarehe ya kuchapishwa.

Matumizi

2.-(1) Amri hii itatumika na-
(a) bandari kavu;
(b) waendeshaji wa magati ya bandari; na
(c) mawakala wa meli.

(2) Bila kuathiri masharti ya aya ya (1), Amri hii haitatumika kwa bandari kavu za kuhifadhi magari.

Tafsiri

3. Katika Amri hii, isipokuwa kama muktadha unahitaji vinginevyo-

Sura ya 415

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania;

"Shirika" maana yake ni Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania lililoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria;

"mpokeaji mzigo" maana yake ni mtu ambaye mzigo umepokelewa kwa niaba yake na kubebwa kwenye meli kwa ajili ya kutumwa kwake na ambaye ametajwa hivyo kwenye hati ya mzigo majini;

"kipindi cha bure" maana yake ni kipindi kinachotolewa na bandari au bandari kavu cha siku za kuhifadhi mzigo kinachoanza tangu tarehe ya mzigo kushushwa melini;

TS. Na. 341 la 2018

"bandari kavu" maana yake ni kituo kinachoweza kutumiwa na yeyote kilicho chini ya usimamizi wa Forodha na kupewa

*Tangazo la Serikali Na. 459 (Linaendelea)*

leseni chini ya Kanuni za Bandari Kavu, 2018;

"bandari kavu ya kuhifadhi magari" maana yake ni bandari kavu ambayo shughuli zake zimejielekeza kushughulikia magari yanayoingizwa nchini;

"utaratibu wa uongezaji wa bandari" maana yake ni mpangilio wa uendeshaji ambapo mwendesha bandari huamua kutoa maagizo kuwa shughuli za upokeaji, uhifadhi na utoaji wa mizigo zifanyike katika bandari kavu na inahusisha uhamishaji wa mizigo hiyo au kasha kati ya maeneo ya bandari kavu yaliyoteuliwa na bandari;

Sura ya 166

"mwendesha bandari" maana yake ni Mamlaka ya Bandari Tanzania iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Bandari;

"mtumaji" maana yake ni mtumaji wa mzigo aliyetajwa katika hati ya mzigo majini;

"utaratibu wa uteuzi wa mtumaji" maana yake ni mpangilio wa uendeshaji wa kuhamisha mzigo kutoka bandarini kwenda bandari kavu iliyotajwa kama itakavyoamuliwa na mtumaji; na

"tozo" maana yake ni gharama au bei pamoja na vigezo na masharti yanayotumiwa na mtoa huduma anayedhibitiwa.

## SEHEMUYA PILI
## TOZO NA MASHARTI YANAYOTUMIWA

Wajibu wa kuzingatia tozo, vigezo na masharti yaliyoidhinishwa

4. Mtu atatumia tozo na vigezo vilivyoidhinishwa kama ifuatavyo:

(a) tozo ya uhamishaji wa kasha kutokana na makubaliano pamoja na masharti mengine endapo ni utaratibu wa uteuzi wa mtumaji utatumika;

(b) kipindi cha bure cha siku tano kwa mzigo wa ndani ya nchi na kipindi cha bure cha siku kumi na tano kwa mzigo unaopita kwenda nchi jirani kwa mzigo uliochukuliwa na mteja kutoka bandarini; na

(c) angalau kipindi cha bure cha siku saba kwa mzigo ya ndani ya nchi na angalau kipindi cha bure cha siku kumi na tano kwa mzigo unaopita kwenda nchi jirani kwa mzigo uliochukuliwa na mteja kutoka bandari kavu.

*Tangazo la Serikali Na. 459 (Linaendelea)*

Uteuzi wa mtumaji au mpokeaji

5.-(1) Mtumaji au mpokeaji mzigo ataruhusiwa kuteua bandari kavu kwa ajili ya kuhamishia mzigo chini ya utaratibu wa uteuzi wa mtumaji.

(2) Endapo uteuzi utafanywa na mpokeaji mzigo, mawasiliano na wakala wa meli yatafanyika kabla ya orodha ya mizigo melini haijawasilishwa ofisi ya Forodha.

Gharama ya uteuzi

6. Wakala wa meli anaweza kutoza kiasi kisichozidi Dola za Marekani kumi kwa hati ya mzigo majini kama gharama ya uteuzi.

Gharama ya uteuzi baada ya kuwasilishwa kwa orodha ya mizigo melini

7.-(1) Endapo mpokeaji mzigo ameteua au amebadilisha uteuzi wa bandari kavu baada ya orodha ya mizigo melini kuwasilishwa ofisi ya Forodha, mwendeshaji wa gati la bandari atamtoza mpokeaji mzigo kiasi cha Dola za Marekani mia moja kwa kila kasha.

(2) Kwa kuzingatia aya ndogo ya (1), wakala wa meli ambaye ameshindwa kuheshimu ombi la uteuzi wa bandari kavu lililowasilishwa na mpokeaji mzigo kabla ya kuwasilishwa kwa orodha ya mizigo melini kwa mujibu wa Amri hili, atalipa gharama ya uteuzi baada ya kuwasilishwa kwa orodha ya mizigo melini.

Uteuzi wa mwendesha bandari kwa niaba ya mpokeaji mzigo

8. Endapo mpokeaji mzigo ameshindwa kuteua bandari kavu kabla ya kuwasilishwa kwa orodha ya mizigo melini kwenye ofisi ya Forodha kwa mujibu wa Amri hili, itakuwa ni ushahidi wa mpokeaji mzigo kuwa amemkasimu mwendeshaji wa gati la bandari kufanya uteuzi huo kwa niaba yake kwa utaratibu wa uongezaji wa bandari.

Gharama za uamishaji chini ya utaratibu wa uongezaji wa bandari

9.-(1) Endapo kasha la ndani ya nchi limeteuliwa chini ya utaratibu wa uongezaji wa bandari, mpokeaji mzigo atatakiwa kulipa tozo ya uhamishaji kasha isiyozidi Dola za Marekani sitini na tano kwa kila kasha.

(2) Endapo kasha linasafirishwa kwenda nchi jirani limeteuliwa chini ya utaratibu wa uongezaji wa bandari, mwendeshaji wa gati la bandari atailipa bandari kavu tozo ya uhamishaji kasha kama itakavyokubaliwa kati ya mwendeshaji gati la bandari na bandari kavu.

*Tangazo la Serikali Na. 459 (Linaendelea)*

Mwendeshaji gati la bandari kuingia mkataba na bandari kavu

10.-(1) Mwendeshaji wa gati la bandari ataingia makubaliano na bandari kavu kwa ajili ya utunzaji wa makasha kwa kuzingatia haki, ikiwa ni pamoja na kiasi kilichokubaliwa cha tozo ya uhamishaji makasha ambayo italipwa na mwendeshaji wa gati la bandari.

(2) Mwendeshaji wa gati la bandari atawasilisha nakala ya makubaliano kwa Shirika ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya Amri hii kuanza rasmi.

Ulipaji gharama ya uhifadhi na mtu atakayewajibika

11. Mtu atakayehusika na ucheleweshaji wa kuhamisha kasha lililoteuliwa kwenda bandari kavu, atalipa tozo zinazohusiana na uhifadhi.

Aina ya makasha yatakayohamishwa kwenda bandari kavu

12.-(1) Bandari itahamisha makasha ya ndani ya nchi kwenda kwenye bandari kavu.

(2) Bila kuathiri aya ndogo ya (1), mwendeshaji wa gati la bandari atahamisha kasha linalopita kwenda nchi jirani lililokaa bandarini muda mrefu zaidi ya kipindi cha bure kwenda bandari kavu kwa gharama itakayolipwa na mpokeaji mzigo.

## SEHEMU YA TATU
## VIWANGO NA GHARAMA CHINI YA UTARATIBU WA UONGEZAJI WA BANDARI

Gharama za uondoshaji

13. Mwendeshaji wa gati la bandari au bandari kavu atatoza Dola za Marekani mia moja kwa kasha lenye ukubwa sawa futi ishirini na Dola za Marekani mia moja hamsini kwa kasha lenye ukubwa sawa na futi arobaini kama malipo ya uondoshaji baada ya kuisha kwa kipindi cha bure.

Malipo ya uhifadhi katika bandari kwa makasha ya ndani

14. Mwendeshaji wa gati la bandari atatoza tozo ya uhifadhi kwa kasha la ndani ya nchi litakalochukuliwa na mteja kutoka bandarini kama ifuatavyo:

(a) Dola za Marekani ishirini kwa kasha lenye ukubwa sawa na futi ishirini na Dola za Marekani arobaini kwa kasha lenye ukubwa sawa na futi arobaini

*Tangazo la Serikali Na. 459 (Linaendelea)*

kutoka siku ya sita hadi siku ya kumi na tano baada ya kipindi cha bure; na

(b) Dola za Marekani arobaini kwa kasha lenye ukubwa sawa na futi ishirini na Dola za Marekani themanini kwa kasha lenye ukubwa sawa na futi arobaini kutoka siku ya kumi na sita na kuendelea baada ya kipindi cha bure.

Malipo ya uhifadhi katika bandari kavu kwa makasha ya ndani

15. Bandari kavu itatoza tozo ya uhifadhi wa kasha la ndani ya nchi kama ifuatavyo:

(a) Dola za Marekani ishirini kwa kasha lenye ukubwa sawa na futi ishirini na Dola za Marekani arobaini kwa kasha lenye ukubwa sawa na futi arobaini kutoka siku ya nane hadi siku ya kumi na tano baada ya kipindi cha bure; na;

(b) Dola za Marekani arobaini kwa kasha lenye ukubwa sawa na futi ishirini na Dola za Marekani themanini kwa kasha lenye ukubwa sawa na futi arobaini kutoka siku ya kumi na sita na kuendelea baada ya kipindi cha bure.

Malipo ya uhifadhi kwa makasha yanayopita kwenda nchi jirani

16. Malipo ya uhifadhi kwa makasha yanayopita kwenda nchi jirani yaliyochukuliwa na mteja kutoka katika bandari au bandari kavu itakuwa kama ifuatavyo:

(a) Dola za Marekani ishirini kwa kasha lenye ukubwa sawa na futi ishirini na Dola za Marekani arobaini kwa kasha lenye ukubwa sawa na futi arobaini kutoka siku ya kumi na sita hadi siku ya ishirini na moja baada ya kipindi cha bure;

(b) Dola za Marekani arobaini kwa kasha lenye ukubwa sawa na futi ishirini na Dola za Marekani themanini kwa kasha lenye ukubwa sawa na futi arobaini kutoka siku ya ishirini na mbili na kuendelea baada ya kipindi cha bure.

Tozo ya ukaguzi wa forodha

17. Bandari au bandari kavu itatoza Dola za Marekani tisini kwa kasha lenye ukubwa sawa na futi ishirini na Dola za Marekani mia moja arobaini kwa kasha lenye ukubwa sawa na futi arobaini kwa ukaguzi wa forodha.

*Tangazo la Serikali Na. 459 (Linaendelea)*

Mabadiliko ya hadhi ya mzigo

18. Bandari au bandari kavu itatoza Dola za Marekani themanini kwa kasha lenye ukubwa sawa na futi ishirini na Dola ya Marekani mia moja thelathini na tano kwa kasha lenye ukubwa sawa na futi arobaini kwa ajili ya mabadiliko ya hadhi ya mzigo.

Fidia kwa ucheleweshaji wa utoaji makasha

19. Bandari au bandari kavu itamfidia mpokeaji mzigo kwa ucheleweshaji wa utoaji kasha endapo mpokeaji mzigo huyo yuko tayari na anataka kupokea kasha kama itakavyoelekezwa na Shirika.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA JUMLA

Mfumo wa ufuatiliaji

20. Mwendesha bandari atatengeneza mfumo wa kielektroniki wa kufuatilia utoaji makasha kupitia bandari kavu.

Uunganishaji mifumo

21. Mwendeshaji wa gati la bandari au bandari kavu ataunganisha mifumo ili kuwezesha ushughulikiaji wa nyaraka za uondoshaji wa mzigo.

Ufutaji wa Amri SMTRA/3/2009

22. Amri ya Tozo ya Muda Mrefu ya Bandari Kavu Na. SMTRA/3/2009 imefutwa.

Dar es Salaam,
17 Juni, 2022

Kaimu Abdi Mkeyenge
*Mkurugenzi Mkuu*